

MZIDI KUENDELEA

1. Bismillah Rahmani,
Ninamuomba Manani,
Awape wote imani,
Wazidi kumkumbuka.
2. Hao wote kina mama,
Waendelelee daima,
Kumsabihi Rahima,
Bila ya kupumzika.
3. Leo nawapa pongezi,
Akina mama azizi,
Msije mkapuuzi,
Kumuabudu Rabuka.
4. Mungu awape imani,
Muondoke vitandani,
Muende msikitini,
Kumuenzi Mtukuka.
5. Abu wangu kwa hakika,
Bahati inamtaka,
Ndoa anazoiweka,
Zajazwa nyingi baraka.
6. Tangu siku za zamani,
Wote wake wanandani,
Hawamuachi Manani,
Kwa nyuso chini kuweka.
7. Zama akikaa nae,
Mama binti Anenae,
Alizidi endelee,
Qahari kumtamka.
8. Naye mama binti Iddi,
Huyu naye alizidi,
Kumkumbuka Wadudi,
Kwenye msala kukaa.
9. Na yeye namuomba,
Azidi kuendelea,
Kumsabihi Jalia,
Aweze kufarijika.
10. Na mama yangu Ramla,
Usimwache akalala,
Bila kudumisha sala,
Kwa kitandani kutoka.
11. Mwisho naye abu wangu,
Mpambe ya ulimwengu,
Na pia Mwenyezi Mungu,
Azidi kukukumbuka.

Hamidu R. Tambwe
MBEYA
Novemba, 1967